JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI

Simu: +255-26- 2323201-7
Nukushi: +255-26-2323208
Barua pepe: nje@nje.go.tz
Tovuti: www.foreign.go.tz

Jengo la LAPF Ghorofa ya 6,
Barabara ya Makole,
S.L.P 2933,
DODOMA.

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

**Maandalizi ya Mkutano wa 18 wa kawaida wa Wakuu wa Nchi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki yakamilika.**

Maandalizi ya Mkutano wa 18 wa Wakuu wa Nchi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki unaotarajiwa kufanyika tarehe 20 Mei, 2017 Jijini Dar es Salaam, Tanzania yamekamilika.

Pamoja na mambo mengine Mkutano huu wa ngazi ya Juu katika Jumuiya unatarajia kufanya mambo yafuatayo;

- Kujadili na kuzingatia masuala mbalimbali kuhusu Mkataba wa Ushirikiano wa Kichumi (EPA) kati ya Jumuiya ya Ulaya na Jumuiya ya Afrika Mashariki
- Taarifa ya namna endelevu ya Uchangiaji wa bajeti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki
- Kizingatia taarifa ya utekelezaji wa hatua ya kuelekea Shirikisho la Kisiasa la Jumuiya ya Afrika Mashariki
- Uteuzi wa Naibu Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kutoka Tanzania
- Uteuzi wa Jaji wa Mahakama ya Jumiya ya Afrika Mashariki kutoka Sudan Kusini
- Kupokea taarifa ya maendeleo ya ushikiriki wa Sudan Kusini katika Jumuiya ya Afrika Mashariki
- Taarifa ya maendeleo ya zoezi la ukaguzi wa suala la Somalia kujiunga katika Jumuiya ya Afrika Mashariki

- Taarifa ya namna ya kuwezesha uundaji wa magari katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na kupunguza uagizaji wa magari yaliyotumika kutoka nje ya Jumuiya

- Taarifa ya mapitio kuhusu sekta ya nguo na ngozi juu ya kuzuia/kuondoa uagizaji wa nguo na viatu vilivyotumika kutoka nje ya Jumuiya

Aidha katika Mkutano huu, Wakuu wa Nchi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wanatarajia kupokea na kuzingatia misuada ya sheria mbalimbali zilizopitishwa na Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki na kutoa tuzo kwa wanafunzi walioshinda shindano la uandishi wa insha la Jumuiya ya Afrika Mashariki. Vilevile Mkutano huu unatarajia kutangaza mabadiliko katika eneo la Elimu ya Juu ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mkutano huu wa Kawaida wa Wakuu wa Nchi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki utatanguliwa na Mkutano wa Dharura wa 34 wa Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki unaotarajiwa kufanyika tarehe 18 Mei, 2017 katika Hoteli ya Serena Jijini Dar es Salaam.

**Imetolewa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini,**
**Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki**
**17/05/2017**